

Nipashhe

Ijumaa Januari 29, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580475



www.twitter.com/nipashetz



www.facebook.com/nipashetz



www.instagram.com/theguardian_newspaper

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US



**Pogba:
Ninafurahia
maisha United**

Mume asakwa
tuhuma kuua
mke kikatili

UKURASA 2



Lori lanaswa
na magunia
80 ya bangi

UKURASA 3

Kauli ya meya kuzuia barakoa yazua jambo

• **Mwenyewe** atoa
msimamo kuhusu uamuzi
wake... *Endelea Ukurasa 2*

RIPOTI MAALUM



**Magufuli
amsamehe
mkurugenzi
aliyenunua
gari la
mil. 400/-**

UKURASA 2

**Wanyama
hawa
marufuku
kwenye
bucha
nyamapori**

UKURASA 3



Meya wa Manispaa ya Moshi, Juma Raibu. Picha: MPIGAPICHA WETU

MICHEZO

GOMES ATEMA CHECHE SIMBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

Mume asakwa kwa tuhuma kuua mke

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamsaka, Samuel James, mkazi wa Mtaa wa Mageuzi, Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, kwa tuhuma za mauaji ya mkewe, Paulina Daudi.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema jana kuwa mauaji hayo yalitokea Januari 26, mwaka huu, saa tatu asubuhi wakiwa nyumbani kwao.

Alisema mwanamke huyo aliuawa na mumewe, baada ya kutokea ugomvi wa kifamilia.

Alisema mtuhumiwa James aliamua kumpiga mkewe ngumi pamoja na mtwangio sehemu mbalimbali za mwili wake na kumsababishia kifo.

“Mwanamke alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, na mwili wake umehifadhiwa katika chumba cha maiti hospitalini hapo,” alisema Kamanda Magiligimba.

Aidha, alisema baada ya mauaji hayo mtuhumiwa alikimbilia kusikojulikana, na kwamba Jeshi la Polisi linamsaka popote alipo, ili akamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kamanda Magiligimba aliwataka wanandoa mkoani Shinyanga, kuacha tabia ya kushambuliana, badala yake likitokea tatizo waende kutafuta suluhu kwenye mamlaka husika, likiwamo dawati la jinsia la jeshi hilo, kabla ya kusababisha madhara.

Kauli ya meya kuzuia barakoa yazua jambo

Na Mwandishi wetu

KAULI ya Meya wa Manispaa ya Moshi, Raibu Juma, kuwaamuru wananchi walioshiriki kikao cha Baraza la Madiwani kuvua barakoa walizokuwa wamevaa, imezua mjadala kwenye mitandao ya kijamii.

Jana, wakati kikao hicho kinaendelea, Meya Juma aliwaona wananchi walioingia kikaoni humo wakiwa wamevaa barakoa na kuwaamuru kuzivua kwa madai kwamba Moshi hakuna ugonjwa wa corona.

Baada ya kusambaa kwa taarifa hizo, mjadala iliibuka kwenye mitandao ya kijamii kuhoji uamuzi huo, huku kukiwa na taarifa za kuwataka wananchi

kuchukua tahadhari kwa kuwa Tanzania si kisiwa na ugonjwa huo umeziathiri nchi za jirani kwa kiasi kikubwa.

“Kama kweli kasema hayo basi hajelewa maana ya barakoa, anahitaji kusaidiwa. Barakoa na sanitizer (vitakasa mikonono) ndiyo kinga. Walio wengi wanaiweza na palipo na hisia au shaka ndiyo silaha ya kwanza,” alisema mmoja wa wachangiaji.

Mwingine aliandika: “Halafu si kwa corona... kuna magonjwa mengine mtu anaweza kujikinga kwa kuvaa barakoa.”

“Kwani barakoa inamzuia nini yeye kama meya kwenye kutekeleza majukumu yake? “Ningekuwa mimi nisingevua na angekuwa na wajibu wa kunipatia kanuni aliyotumia

kukataza barakoa, kikao kingevurugika,” alisema mchangiaji mwingine.

“Duh kwani kuvaa barakoa ni jinai au ni kinyume cha kanuni?” Alisema mchangiaji mwingine na kuongeza kuwa: “Eti yeye hajavaa, hivyo nao wasivaa, kwa hiyo kwa vile yeye huwa hatumii ‘condom’ na wajumbe wote wa baraza wasitumie? Alihoji.

Katika ukurasa wa twitter, baada ya kurushwa kwa taarifa hiyo maoni ya wasomaji yalikuwa kama ilifuatavyo.

“Muache ngoja tuone mwisho wake, shemasi tupe na jina lake kabisa huyo meya ili nisave (nihifadhi) kwa kumbukumbu. Nipo msibani nimevaa aelekezwe nilipo, nipo msibani Sanya Juu,” aliandika mwananchi

mmoja akiwa ameambatanisha picha yake amevaa barakoa.

“Meya wacha nimwache kwanza. Ila walioambiwa wavue na wakavua hao ndiyo... ulikozaliwa, kukulia, kulelewa na haujafa unaamrisha na mwanadamu mwenzako kutochukua hatua dhidi ya magonjwa kisa yeye ni kiongozi kwa cheo,” alihoji.

“Issue (jambo) ya kuchukua tahadhari ingefaa zaidi serikali itangaze iwe ni utaratibu wa watu wote kuvaa barakoa na kunawa mikonono. Utaratibu wa mtu mmoja kuvaa barakoa kati ya 20 au zaidi bado nachelea kusema ni changamoto kuiwepa korona hata kwa hiyo moja,” alisema.

Akizungumza na Nipashe, Meya Raibu alisema aliingia kwenye kikao cha baraza ambacho kilishafanyika siku mbili zilizopita na hakuna aliyevaa barakoa.

“Kwenye kikao asilimia 98 walikuwa hawajavaa barakoa na ghafla wakaingia wageni watano wamevaa barakoa. Ilikuwa taharuki maana watu walikuwa hawasiliki kikao na wahasika walikuwa wanazitoa wanazishika, wanazivaa juu ya kidevu na chini ya kidevu, ndiyo nikaamuru wazivue,” alisema.

Raibu alisema wananchi wao walivyohojiwa walisema walipata taarifa kuwa corona imesambaa sana Kenya ndiyo maana wakaona wavae barakoa.

“Tulianza kikao tangu asubuhi na hakuna aliyekuwa na tatizo, lakini wao wanavaa barakoa. Moshi ni salama na hadi sasa hakuna tatizo na hakuna corona na kama kuna jambo lolote tutawajulisha wananchi wetu,” alisema.

“Wako madiwani karibu 30, wapo viongozi wa serikali na viongozi wa vyama walioalikwa wote hawa hawajavaa barakoa hata mmoja, lakini limekuja kundi la watu wamevaa barakoa jambo ambalo wanaamini halmashauri hii ina corona, mimi nimewaambia wavue na wamevua,” alisema na kuongeza:

“Nimewaambia wavue waendele kuamini kuwa corona ipo, lakini na tuendeleo kujikinga lakini Manispaa ya Moshi haina corona, tuendeleo kujikinga katika mambo mengine ila tusitiane hofu, katika baraza langu la manispaa sitaruhusu mtu yeyote kuingia na barakoa katika kikao changu kwani ninaamini tuko salama salmini.”



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akishuhudia utiaji saina ya maelewano (MoU) kuhusu mpango mkuu wa ujenzi wa bandari na mji wa kisasa Mangapwani na Bumbwini Zanzibar. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Amour Hamil Bakari pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwekezaji Oman (OIA), Sheikh Mohammed Al Taooqi, katika ikulu ya Zanzibar. Picha: IKULU.

JPM amsamehe mkurugenzi aliyenunua gari la kifahari

Na Waandishi Wetu

RAIS John Magufuli ameipongeza Halmashauri ya Kahama Mji kwa kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda huku akimsamehe mkurugenzi wake, Anderson Msumba, aliyekuwa akikabiliwa na tuhuma za kununua gari la Sh. milioni 400.

Rais alitangaza msamaha huo jana wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha vinywaji baridi na vifungashio cha KOM kina-chomilikiwa na mwekezaji mzawa, Mhoja Nkwabi, eneo la Chapulwa wilayani Kahama.

Alisema kuwa hakuamini kiwanda hi-

cho kama kinamilikiwa na Mtanzania kwa kuwa mara nyingi viwanda vikubwa kama hicho vinamilikiwa na watu kutoka nje.

Rais Magufuli alisema uamuzi wa Halmashauri ya Kahama Mji kutoa eneo kwa ajili ya uwekezaji lenye ekari 60 unapaswa kuigwa na halmashauri zote nchini.

“Nimeipongeza Halmashauri ya Kahama Mji kutoa ardhi bure kwani wanajua faida yake wakitoa ardhi mwekezaji akawekeza, watakusanya mapato, watu watapata ajira, kweli ubunifu huu ni mzuri na kiwanda hiki ninasikia kitaanza mwezi Julai, hivyo upatikane umeme wa uhakika,” aliagiza.

Rais Magufuli alisema pamoja na kutuhumiwa kwa kashfa mbalimbali, iki-

wamo matumizi makubwa ya fedha, makosa aliyofanya mkurugenzi huyo ya-mefutwa na akili yake katika kuiboresha Kahama.

“Nimeamua kumsamehe mkurugenzi huyu, na hili gari ninamrudishia aendeleo kuliendesha, lakini asirudie tena kununua magari nje ya utaratibu wa sheria.

“Ninasema kwa dhati, sitaki kuwa mnafiki, amefanya makubwa, mkurugenzi hongera sana!” Rais Magufuli alisifu.

Rais Magufuli alitumia mamlaka yake kuipandisha hadhi Kahama na kuwa Manispaa kuanzia jana, baada ya kuridhishwa na kasi kubwa ya maendeleo ya mji huo na kukidhi vigezo vya hadhi ya manispaa.

Alisema Wilaya ya Kahama sasa inachangia asilimia 50 ya mapato ya mkoa wote wa Shinyanga, huku ikijitegemea kwenye uendeshaji wa miradi.

Kiongozi huyo wa nchi alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, kuipatia halmashauri hiyo Sh. milioni 500, ili ikamilishe ujenzi wa hospitali.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha KOM, Mhoja Nkwabi, alisema mazingira rafiki ndiyo yamemvutia kuwekeza wilayani Kahama, akibainisha ujenzi wa kiwanda hicho umegharimu Sh. bilioni 147, akitarajia kutoa ajira za moja kwa moja 400 na 1,000 zisizo za moja kwa moja.

HABARI KITAIFA

RIPOTI MAALUM

Wanyama hawa marufuku kwenye bucha nyamapori

Na Godfrey Mushi, ARUSHA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), imesema tathmini iliyofanya baada ya kutangazwa kuanzishwa kwa bucha za nyamapori, imebaini kuna ombwe la uelewa juu ya biashara hiyo.

Vilevile, mamlaka hiyo imebainisha wanyamapori ambao hawaruhusiwi kuwindwa na kuuzwa katika bucha hizo ni wale walio hatarini kutoweka, wakiwamo tembo na faru na kwamba wanaoruhusiwa ni kwa ajili ya kitoweo ni wanyama aina 20, tofauti na zile aina 88 za uwindaji wa kitalii.

Naibu Kamishna wa Utalii, Huduma za Biashara na Utalii wa TAWA, Imani Nkuwi, alibainisha hayo jana alipozungumza jijini Arusha jana na wadau wa biashara ya nyamapori nchini, wawindaji bingwa wa kitalii, wenye mashamba ya nyamapori, wawindaji wa kitoweo na wenye bucha.

Alisema wengi wa waliochangamkia fursa hiyo kwa kuandika mpango wa biashara, waliandika tu bila kufanya utafiti mzuri wa upatikanaji wa vyanzo.

Alisema ili kuondoa ombwe hilo, hivi sasa unafanyika utafiti wa kisayansi, unaohusisha kamati ya wanazuoni kutoka vyyo vitano vinavyofundisha taaluma ya wanyamapori.

Wanazuoni hao wanakuja na tathmini ya kina inayoangalia idadi ya wanyama, uwezo wa wanyama kuzaa, mazingira yao ya asili yapo au yamepungua na

yamepungua kwa kiasi gani na watapendekeza mgao wa taifa wa kuwindwa wanyama.

Naibu Kamishna Nkuwi alisema: "Kwa sababu kuna vitabu vilitolewa vinane na akaandika mimi nitawinda hapa, lakini hakufanya utafiti mzuri, na vilevile hii ni biashara kama zilivyobiashara nyingine ambazo ukitaka kuifanya lazima tufanye utafiti wa kina.

"Sasa huu uelewa kwa wale walioandika mpango biashara, ulikuwa ninadhani ndiyo ombwe lenyewe, ambalo tunalijadili kwa pamoja ili kuboresha hiyo mpango biashara, namna kipekee ambayo ni muhimu sana baada ya hapo, ni kujua kama wewe umefungua bucha ni kuwaambia Watanzania watapata nyama kila baada ya muda gani.

"Kwa sababu kwenye uwindaji wa kitalii, kwa mfano siyo lazima uchukue nyama. Kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia uwindaji wa kitoweo, ziko aina 20, kuna nyati, pofu, kongoni, swala na kadhalika.

"Sasa, wanyama ambao hawaruhusiwi na hatujawajumuisha katika orodha ya wanaotakiwa kuwindwa ni wale ambao wako hatarini kutoweka, kwa mfano tembo, faru," alifafanua.

SHIDA ILIPO

Katika mkutano huo, Naibu Kamishna Nkuwi anafafanua zaidi akisema: "Mtu anachukua kibali anatarajia anakwenda porini na atafika tu pale atakuta wanyama ataanza kuwashughulikia, kumbe uwindaji ni kwenda porini kutafuta.

ITAENDELEA KESHO

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)



UFAFANUZI WA TAARIFA KWA WAAGIZAJI WA MAGARI KUTOKA NJE YA NCHI

2021-01-29

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kutoa ufafanuzi kuhusiana na taarifa iliyotolewa tarehe 2021-01-21 juu ya ukaguzi wa magari kutoka nje ya nchi.

Tunapenda kufafanua kwamba, kwa sasa TBS inaendelea kukagua magari kutoka nje ya nchi kupitia mawakala watatu (3) walioko Japan na mmoja (1) Dubai mpaka pale mikataba yao itakapokoma tarehe 28 Februari, 2021.

Hivyo, Shirika litaendelea kuvitambua vyeti vyote ambavyo vitatolewa na mawakala tajwa ambao maombi yao yatakuwa yamepelekwa na kulipiwa kwa mawakala hao kabla ya tarehe 01 Machi, 2021. Vyeti hivyo vitatambulika mpaka pale vitakapokwisha muda wake ambao ni miezi mitatu (3) tangu tarehe ya cheti kutolewa.

Aidha, Shirika halitatambua vyeti vyote ambavyo maombi yake yatakuwa yamepelekwa kwa mawakala baada ya tarehe 28 Februari, 2021.

Shirika linaendelea kusesitiza kwamba kuanzia tarehe 01 Machi, 2021, utaratibu wa kukagua magari kutoka nje ya nchi utafanyika baada ya kuwasili hapa nchini (Destination Inspection) na waagizaji wote watatakiwa wapeleke maombi TBS na si kwa mawakala.

Waagizaji wanashauriwa kutuma maombi yao wakiambatisha, pamoja na nyaraka nyingine, vyeti vifuatavyo: Certificate of Cancellation, Certificate of Registration, Radiation free certificate na Export certificate.

ANGALIZO: Magari yatakayotoka Japan na Dubai kabla ya ukomo wa mkataba na kuwasili nchini baada ya ukomo wa mikataba bila cheti cha CoC yatatozwa faini (penalty).

Kwa taarifa zaidi usisite kuwasiliana na: -
Mkurugenzi Mkuu,

Shirika la Viwango Tanzania (TBS),
S.L.P. 9524,
Dar-es-Salaam.

Simu: +255(022)2450298/Hotline: +0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz/Tovuti: www.tbs.go.tz
malalamiko @tbs.go.tz

Loli lanaswa na magunia 80 ya bangi

Na Samson Chacha, TARIME

WATU watatu akiwamo dereva wa lori aina ya Scania namba za usajili T 465 DQJ na tela lake namba T 143 DEM, Salum Issa na utingo wake wamekamatawa wakiwa na lori likiwa na magunia 80 ya bangi kavu.

Magunia hayo yaliyokuwa yamechanganywa na magunia 95 ya mahindi mabichi yakisafirishwa kutoka Kijiji cha Nyamwigura kwenda Dar es Salaam.

Dereva huyo ni mkazi wa Nzega mkoani Tabora, alikuwa na utingo wake, Khalid Yusuf, mkazi wa Mwanza pamoja na msindikizaji wa mzi-go huo, Amos Chacha, mkazi wa Mtaa wa Mkuyuni mjini Tarime.

Kamanda wa Polisi Tarime/Rorya, William Mkonda, alisema kuwa Januari 27, mwaka huu Jeshi la Polisi lilipata taarifa kutoka kwa msiri wake kuhusiana na kuonekana kwa lori hilo katika Kijiji cha Nyamwigura likiwa limebeba magunia ya dawa ya bangi.

Kamanda Mkonda alisema baada ya taarifa hiyo, polisi walianza kulifuatilia

na kwamba walilikamata katika Kijiji cha Gamasara na kuliamuru kwenda Kituo cha Polisi Tarime.

Kwa mujibu wa Mkonda, baada ya kukaguliwa na kufunguliwa turubai iliyokuwa imeyafunika

magunia hayo, yalikutwa magunia 80 yaliyokuwa yamefungwa kwa gundi ambayo yalikuwa na dawa za kulevya aina ya bangi pamoja na magunia 95 ya mahindi mabichi yaliyokuwa yamewekwa juu ya magunia hayo.

"Tunawashikilia na tunawahoji kisha tutawafikisha mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili," alisema Kamanda Mkonda.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri, aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo vya usalama kuhusu vitendo vya uhalifu wakiwamo watu wanaojihusisha na kilimo cha bangi.

Aliwataja wengine ni wajasiriamali wanaotumia kemikali pamoja na maofisa biashara, maofisa wa serikali wanaohusika kudhibiti kemikali za dawa za kulevya.



TPB BANK PLC

UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA (HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| TPB BANK PLC WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA, 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | |
|--|---------------------------------------|--------------------------------|--|
| | Robo Mwaka ya /Mwaka wa 31/12/2020 | Robo Mwaka/Mwaka 30/09/2020 | |
| A. MALI | | | |
| 1 Fedha Taslimu | 41,717 | 38,188 | |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 18,324 | 56,064 | |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 100,455 | 143,224 | |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 92,983 | 32,887 | |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 5 | 208 | |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - | |
| 7 Bili Zilizozitakiwa | - | - | |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 85,791 | 82,313 | |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 616,512 | 627,499 | |
| 12 Mali Nyingine | 57,613 | 63,305 | |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - | |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - | |
| 15 Mali Zilizohamishika, Mitambo na Vifaa | 22,951 | 22,285 | |
| 16 JUMLA YA MALI | 1,036,351 | 1,065,973 | |
| B. DHIMA | | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - | |
| 18 Amana za Wateja | 665,496 | 700,578 | |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - | |
| 20 Amana Maalumu | 50,742 | 66,047 | |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 5,915 | 4,664 | |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2 | 85 | |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitatokolewa | 28,505 | 20,138 | |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | |
| 26 Mapato yaliyoingine ya Kipindi Kijicho na Tozo Nyingine Zitatokolewa | 2,825 | 2,671 | |
| 27 Dhima Nyingine | 94,408 | 20,836 | |
| 28 Madeni | 84,293 | 124,334 | |
| 29 JUMLA YA DHIMA | 932,186 | 939,356 | |
| 30 MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29) | 104,165 | 126,619 | |
| C. FEDHA ZA WANAHISA | | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 | |
| 32 Akiba ya Mtaji | - | - | |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | 60,601 | 60,601 | |
| 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 4,488 | 13,214 | |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | 11,004 | 24,732 | |
| 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - | |
| 37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA | 104,165 | 126,619 | |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | - | - | |
| 39 Mikopo Chechefu | 95,781 | 94,642 | |
| 40 Tongo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 17,370 | 36,361 | |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | 44 | 38 | |
| D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.05% | 11.88% | |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 15.00% | 13.88% | |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 95.97% | 97.31% | |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 59.49% | 58.87% | |
| (v) Uwiano wa Mali Zinzozalisha na Jumla ya Mali | 79.02% | 79.51% | |
| (vi) Ongezeko la Amana | -5.01% | -1.09% | |
| (vii) Ongezeko la Mali | -2.78% | 3.84% | |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | | |
|---|-----------------------|---|-------------------------------|---|
| | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
| | 31/12/2020 | 31/12/2019 | 31/12/2020 | 31/12/2019 |
| 1 Mapato ya Riba | 29,845 | 24,717 | 119,266 | 100,178 |
| 2 Gharama za Riba (1 kutoa 2) | (10,179) | (6,615) | (37,675) | (22,496) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 19,666 | 18,102 | 81,591 | 77,683 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (14) | (374) | (372) | (1,100) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tongo katika Mikopo | (3,033) | (2,353) | (8,361) | (10,444) |
| 6 Mapato Yasiyo ya Riba: | 11,948 | 9,585 | 32,845 | 29,642 |
| 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 1,600 | 1,195 | 5,341 | 4,491 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,135 | 4,297 | 14,796 | 14,772 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 6,213 | 4,093 | 12,708 | 10,379 |
| 7 Gharama Zisizo za Riba: | (29,389) | (18,730) | (88,062) | (71,972) |
| 7.1 Mishahara na Maifao | 11,198 | 8,178 | 39,678 | 32,799 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 5,314 | 1,486 | 9,058 | 4,354 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 12,877 | 9,066 | 39,327 | 34,819 |
| 8 Faida/(Hasara) ya Uendeshaji | (822) | 6,230 | 17,641 | 23,809 |
| 9 Tongo la Kodi ya Mapato | 7,904 | 1,725 | 13,153 | 6,900 |
| 10 Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | (8,726) | 4,505 | 4,488 | 16,909 |
| 11 Mapato Mengine Yaliyomuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 Jumla ya Faida (Hasara) Iliyomuishwa kwa | (8,726) | 4,505 | 4,488 | 16,909 |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,039 | 926 | 1,039 | 926 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (311) | 160 | 602 | 602 |
| 15 Idadi ya Matawi | 43 | 38 | 43 | 38 |
| BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.87% | 0.72% | 0.51% | 2.87% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -7.34% | 4.57% | 3.94% | 18.40% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 70.32% | 54.60% | 57.89% | 55.44% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinzozalisha | 2.40% | 3.42% | 11.34% | 15.55% |
| Tarakimu za wastani zitakotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho. | | | | |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA, 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | | |
|--|------------------------------------|--------------------------------------|--|--|
| | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-19 |
| I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (822) | 6,518 | 17,641 | 23,006 |
| Marekebesho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 8,551 | 4,895 | 37,313 | 13,756 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 10,986 | (24,281) | (195,919) | (9,325) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | 2 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (50,386) | (7,686) | 280,794 | 51,578 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | (32,321) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 123,373 | 20,268 | 49,502 | (4,417) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 10,691 | 19,742 | (26,924) | 3,271 |
| - Kodi Iliyolipwa | (1,700) | (6,949) | (6,900) | (6,900) |
| - Mengineyo (bainisha) | 4,601 | 33,939 | (3,742) | 560 |
| Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | 105,295 | 51,694 | 151,717 | 39,210 |
| II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli | | | | |
| Gawio Liliopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,012) | (1,459) | (4,581) | (5,411) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | 1 |
| Ununuzi wa Amana Zilizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | (2,012) | (1,459) | (4,581) | (5,410) |
| III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli | | | | |
| Ujipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Liliolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | (1,210) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 888 |
| Mengineyo (bainisha) | (1,428) | (1,148) | (5,981) | (4,992) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | (1,428) | (1,148) | (5,981) | (5,314) |
| IV: Fedha Taslimu na Mali Zinzozalisha na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinzozalisha na Fedha Taslimu | 101,854 | 49,087 | 141,154 | 28,486 |
| Fedha na Mali Zinzozalisha na Fedha Taslimu | 73,046 | 23,959 | 33,746 | 5,260 |
| Mwanzoni mwaka Robo Mwaka/Mwaka | 174,900 | 73,046 | 174,900 | 33,746 |
| Mwishoni mwaka Robo Mwaka/Mwaka | | | | |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | | | | | |
|--|---------------|---------------------------------|-------------------------|----------------------|----------------------------|---------------|----------------|
| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tongo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
| Mwaka wa sasa | 28,072 | - | 60,601 | - | - | 10,220 | 98,893 |
| Salio la mwanzo wa mwaka | - | - | - | - | - | - | - |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 4,488 | 4,488 |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Liliolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | 784 | - | 784 |
| Salio la mwisho wa mwaka | 28,072 | - | 60,601 | - | 784 | 14,708 | 104,165 |
| Mwaka uliopita | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 28,072 | - | 40,539 | 135 | 3,913 | 10,262 | 82,920 |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | 4,048 | (135) | (3,913) | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 15,891 | - | - | - | 15,891 |
| Mapato mengine yaliyomuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tongo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Liliolipwa | - | - | (1,210) | - | - | - | (1,210) |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofanuliwa | - | - | 133 | - | - | - | 133 |
| Kurudishwa Gawio Liliomamishwa | - | - | 1,200 | - | - | - | 1,200 |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (42) | (42) |
| Salio la mwisho wa mwaka | 28,072 | - | 60,601 | - | - | 10,220 | 98,893 |

BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA, 2020

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaji ni zilele zilizotumika wakati wa uandaji wa Taarifa za Fedha zilizozalishwa za mwaka uliopita (kama kujiua na mabadiliko katika sera za uandaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yalelewe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|--|------------|------------|
| MR. SABASABA K. MOSHINGI (Ofisa Mtejaaji Mkuu) | IMESAINIWA | 27.01.2021 |
| MS. REGINA E. SEMAKAFU (Mkuu wa Fedha) | IMESAINIWA | 27.01.2021 |
| MR. ANUARY KITEMANGU (Kaimu Mkuu wa Ndani) | IMESAINIWA | 27.01.2021 |

Sisi ulioitaja hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatarika kwamba tumezidhimini taarifa hizi na kwa ulewa na imani yetu kubwa zimeandajiwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uandaji wa Taarifa za fedha na matakiwa ya sheria ya Benki na Taasisi za Fedha za mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|--|------------|------------|
| DR. EDMUND B. MNDOLWA Mwenyekiti wa Bodi | IMESAINIWA | 27.01.2021 |
| MS. ANNE C. MBUGHUNI Mjumbe wa Bodi | IMESAINIWA | 27.01.2021 |



TPB BANK MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|-----------------------------------|---|--|
| Minimum Opening Balance | Quick Account | 20,000 |
| | Salary Account | FREE |
| | Platinum Account | 15,000 |
| | Call Account | 100,000 |
| | Minor Account | 20,000 |
| | Scout Minor | 10,000 |
| | Scout | 30,000 |
| | WADU | 20,000 |
| | YANGA VIP Card | 1,200,000 |
| | YANGA Member Card | 25,000 |
| Bank Statement | Group Account | FREE |
| | | Within a month it is FREE and more than a month is 1500 per document |
| Monthly Maintenance Fee | Savings Account | 1,560 |
| | Platinum Account | 1,560 |
| | WADU Account | FREE |
| | Call Account | 6,500 |
| | Minor Account | FREE |
| | Group Account | FREE |
| | | |
| Dormant Accounts Fee | 1 year to 5 years | 1,300 |
| | 6 years to 10 years | 5,000 |
| | 11 years to 15 years | 10,000 |
| Activation of Dormant Account | | FREE |
| ATM Charges | ATM Balance Enquiry- All cards | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Cash Withdraw on TPB ATMs | 1,300 |
| | Cash Withdraw on other UMOJA SWITCH ATM | 1,300 |
| POS Branches | Balance Enquiry | 150 |
| | Mini statement | 150 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | 2,600 |
| POS Agents | Balance Enquiry | 100 |
| | Mini statement | 200 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| Mobile Banking | POS Withdraw | see Tiered Fees 1 |
| | Balance Enquiry | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Full Statement | 400 |
| | Pin Charge | FREE |
| | Notification /Alert | 250 |
| | Account Transfer | FREE |
| | Mobile Agent Deposit | 200 |
| | Mobile Agent Withdraw | see Tiered Fees 2 |
| | Mobile Money to Bank Deposit | 1,300 |
| Closing Account | | 13,000 |
| FDR Min. Opening Balance | | 100,000 |
| ATM Issuance and Replacement Fees | Pipote Card | 15,000 |
| | Yanga Member card | 20,000 |

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|--|---|----------|
| Other ATM & Normal Card | Pin Re-issue | FREE |
| | Collection of ATM card at Non Domicile Branch | 6,500 |
| | Uncollected and destroyed ATM card | 6,500 |
| | First ID card (Local and Foreign Currency) | 4,000 |
| | Replacement Of ID card | 2,600 |
| Cash withdraw | Teller withdraw upto 10,000,000 | 2,600 |
| | Teller withdraw from 10,000,001 to 50,000,000 | 5,000 |
| | Teller withdraw from 50,000,0001 to 100,000,000 | 15,000 |
| | Teller withdraw above 100,000,001 | 30,000 |
| | Cheques Clearing Fee | 3,000 |
| | Special Clearance | 50,000 |
| | Dishonoured Cheque | 35,000 |
| | TISS Inwards | FREE |
| | TISS- Outward | 10,000 |
| | Within the Bank | 1,300 |
| To other Banks | 13,000 | |
| POS Withdraw & Money Transfer/ Tansit fees | POS Withdraw | Tiered 1 |
| | 0-10,000 | 800 |
| | 10,000.01-20,000 | 1,250 |
| | 20,000.01-50,000 | 1,500 |
| | 50,000.01-100,000 | 2,250 |
| | 100,000.01-200,000 | 2,750 |
| | 200,000.01-300,000 | 4,200 |
| | 300,000.01-400,000 | 5,500 |
| | 400,000.01-500,000 | 6,000 |
| | 500,000.01-700,000 | 6,500 |
| | 700,000.01-2,000,000 | 7,500 |
| | TPB Mobile Transfer Fee | Tiered 1 |
| | 500-10,000 | 850 |
| | 10,000.01-50,000 | 1,200 |
| | 50,000.01-100,000 | 1,500 |
| 100,000.01-250,000 | 2,800 | |
| 250,000.01-500,000 | 4,600 | |
| 500,000.01 - 750,000 | 7,500 | |
| 750,000.01 - 1,000,000 | 10,000 | |
| Tiered 2 | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

RATES AND CHARGES FOR USD ACCOUNT

| | | |
|---------------------|--------------------------------|--------------------------|
| Maintenance Fee | Savings Account | 1 |
| | Call Account | 5 |
| Deposit Fee | Non Account Holder | Free |
| | | |
| Opening Balance | | 50 |
| Account closure fee | | 10 |
| Bank Statements | | Free |
| | Balance Enquiry- Banking Hall | Free |
| | Confirmation letter | Free |
| Withdraw Fees | Below 50 | 1 |
| | 51-1,000 | 2.5 |
| | 1,001-2,250 | 5 |
| | 2,251-5,000 | 15 |
| | Above 5,000 | 0.25% |
| | | 1.3 USD (TZS Equivalent) |
| Cheque | Any amount | 40 |
| | Special Clearance | 40 |
| | Unpaid cheques-Refer to Drawer | 10 |
| | Special Payment | 20 |
| Dormant | Dormant Account Fee | 5 |
| | Re-Activation | Free |
| TISS | | 10 |



+255 787 669 977

tpbbank//facebook

tpbbank//instagram

www.tpbbank.co.tz

LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

1. FEES ON CONSUMER LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE | S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|-----|----------------------------------|--|-----|-------------------------|--|
| 1. | Consumer Loan Administration Fee | 1.5% of the Approved Loan. Minimum TZS. 10,000/= | 2. | Loan Application Fee | TZS. 10,000/= |
| | | | 3. | Loan Administration Fee | 1.5% Minimum. TZS. 10,000/= Maximum TZS. 100,000/= |

2. FEES ON WASTAAFU LOANS

3. OTHER CHARGES ON INDIVIDUAL MICRO CREDIT

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|-----|--|----------------------------|
| 1. | MIC Loan Application Fee | TZS. 20,000/= |
| 2. | MIC Loan Processing/Administration Fee | 1.5% Minimum TZS. 50,000/= |

4. INTEREST RATES AND OTHER CHARGES ON BUSINESS LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|-----|---|-----------------------------|
| 1. | Loan Application Fees for Business and Personal Loans | TZS. 50,000/= |
| 2. | Loan Administration Fee - Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount |



Pata Zaidi

Wekeza kuanzia

TZS. Milioni 5

Kwa miaka 2

Upute Riba ya

11%

Kwa mwaka



Huduma kwa Witoja: +255 787 66 9977 www.tpbbank.co.tz

Nipashe

MWANGA WA JAMII

Ngorongoro sasa haihitaji siasa tena

MAMLAKA ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA), imeeleza hali halisi ya ongezeko la watu, mifugo na shuguli za kibinadamu ambazo zimeufikisha uhifadhi katika hali ngumu na kuongezeka kwa migogoro kati ya wanyamapori na binadamu.

Wakati wa kuanzishwa kwa mamlaka hiyo mwaka 1959 kukiwa na watu 8,000, sasa wamefikia zaidi ya 200,000 na malaki ya mifugo, ambayo asilimia 80 inamilikiwa na asilimia 20 ya wakazi.

Tayari timu ya wataalamu imeshaanza kuangalia namna ya kuendeleza eneo hilo lenye hadhi nne za urithi wa dunia, imekusanya maoni ya namna matumizi mseto ya eneo hilo yanaweza kufanyika hasa kwa kuwa na kanda za matumizi.

Mbaya zaidi hali ya umaskini katika eneo hilo ni ya kutisha kwa kuwa sheria hairuhusu shughuli zozote nje ya ufugaji, na licha kuwa na shule 25 za msingi na mbili za sekondari, lakini bado kiwango cha kutojua kusoma na kuandika ni asilimia 64.5.

Wataalamu wanasema imefika mahali kwamba kila jitihada za uhifadhi zinazofanyika zinaathari kwa wananchi wanaoishi ndani ya Ngorongoro, na kila shughuli ya kibinadamu inayofanyika ina athari katika uhifadhi.

Aidha, kutokana na mabadiliko ya maisha wananchi hao wanaachana na kutegemea mifugo kwa ajili ya chakula na sasa wanataka kulima mazao mengine, huku wengi wakiachana na ujenzi wa nyumba za asili na kujenga za kisasa za bati ambazo haziruhusiwi, na mwisho wanaingia katika mgogoro na mamlaka.

Pia kuna changamoto kubwa ya wanyama kula mifugo, magonjwa ya kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na wanyama wafugwao, jambo ambalo ni hatari sana na kadri watu wanavyoongezeka eneo hilo linashindwa kutosheleza mahitaji.

Umuhimu wa watu katika eneo hilo na uhifadhi ndiyo upekee wa Ngorongoro yenye historia ya binadamu wa kwanza, na watu hutoka maeneo mbalimbali duniani kujionea maajabu ya binadamu kuishi na wanyamapori kama Simba, tembo, faru, nyati, Twiga na wengine.

Kilio cha wataalamu ni muhimu sana likafanyiwa kazi, kwa hali iliyofikia hakuna namna ambavyo Ngorongoro inaweza kuendelea na idadi hiyo ya watu. Ni lazima ufanyike utaratibu wa kupunguza watu kama ilivyofanyika miaka ya nyuma kwa kaya zaidi ya 119 zenye watu zaidi ya 500 ziliondolewa na kwenenda kuanza maisha nje ya hifadhi.

Mbaya zaidi hali siyo njema sana hasa kuwapo kwa mimea vamizi ndani ya hifadhi yakiwamo magugu maji ambayo yanapunguza mimea ya asili inayotegemewa na wanyama kwa ajili ya chakula.

Kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu na mabadiliko ya tabianchi, sasa vyanzo vya maji vimepungua kiasi cha wanyama kukosa maji na kuyatafuta nje ya hifadhi, ambayo hatari yake ni kuongezeka kwa migogoro kati ya wanyama na binadamu, hivyo majangili kutumia mwanya huo kuu wanyama.

Ni lazima maamuzi magumu yafanyike Ngorongoro ili kunusuru uhifadhi na kuendelea kupata mabilioni ya fedha yanayotokana na utalii, vinginevyo taratibu eneo hilo litakuwa historia.

Ni muhimu sana wananchi wakashirikishwa na wale ambao wako tayari kuondoka na kuanza maisha nje ya hifadhi kuruhusiwa kufanya hivyo, pasipo kuwapo kwa shinikizo la wacheache ambao inaelezwa ni wanufaika.

Kwa ujumla suala la Ngorongoro halihitaji siasa, bali kuangalia uhalisia wa mambo ya kuchukua hatua, lakini kama siasa itapelewa kipaumbele basi kidogo kidogo tuanze kuisahau Ngorongoro.



Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

Mengi yaliyoahidiwa yanahitajika kupabadili maisha 'Uwanja wa Fisi'

KAMA ilivyo miji mingine mikubwa, Dar es Salaam nayo imegawanyika katika kanda ndogo ndani yake, kuna makazi yaliyogawanyika kwa wenye vipato vya ngazi tofauti; vikubwa, vya uwezo wa kati kiuchumi na walalaho.

Jijini Dar es Salaam, kuna mahali maarufu kwa jina la 'Uwanja wa Fisi' eneo lililoko kati ya Manzese na Tandale. Ni miongoni mwa makazi yanayoangukia sifa ya wanaoishi walalaho.

Hapo kunasifika kwa wakazi wake wengi wana uchumi katika kiwango duni, mlo wao wa uhakika na daraja la chini zaidi.

Asilimia kubwa ya wakazi wa 'Uwanja wa Fisi' wamefikia hatua, lindi la umaskini wao ni wa kushindwa kumudu gharama za maisha, ikiwamo kununua chakula na mavazi. Malazi yao yalivyo.

Ni hali inayowalazimisha kununua vyakula vya bei nafuu na wakazi wanalazimika kununua vitu ambavyo muda wake wa matumizi umeisha. Kikubwa hapo hata kufikia uamuzi huo, ni kusaka unafuu wa maisha.

Mtu anapoenda katika maduka mbalimbali, wafanyabiashara wa maeneo yao nao wanauza bidhaa zao kulingana na hali halisi ya maisha ya wakazi, ili wafanikishe mauzo.

Kwa mfano, katika maduka yaliyopo 'Uwanja wa Fisi' panapatikana sukari, chumvi, majani ya chai na vingine vinapimwa na kufungwa katika karatasi, mafuta ya kula nayo yakiwa na vipimo vyake vidogo, vina vyopatikana kwa bei nafuu. Zote ni jitihada za kuwafikia wateja wanakojimudu kiuchumi.

Hiyo haimaanishi mwenye uwezo wa kupimiwa sukari katika mzani, hatafanyiwi hivyo, la hash! Nafasi yake nayo ipo, kila anayetaka huduma anapata.

Kumekuwapo ahadi mbalimbali za kubadili 'Uwanja wa Fisi' kuwa bora zikilenga kukomesha shughuli zote, ambazo si halali, ambazo hufanyika katika eneo hilo, lakini hazijitimia.

Miongoni mwa ahadi hizo ni ile ya aliyekwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alipotembelea Uwanja wa Fisi na akaahidi azma ya nyumba za mahali hapo kubomolewa, ili kupageuza kuwa ukanda

wa biashara.

Nakumbuka Novemba mwaka 2016, Makonda aliahidi azma ya nyumba zote katika eneo hilo kubomolewa na kuwapa watu waendeshe viwanda vidogo. Aliahidi hatua ya kwanza muhimu ni kufanyika tathmini, ili wenye nyumba walipwe chao.

"Nimejionea hali ilivyo katika maeneo ya Mtaa wa Fisi, si mazuri. Nitatafuta wafanyabiashara wa viwanda wanunue eneo hili, (wakazi) walipwe fedha zao wapishe eneo hili," anasema Makonda.

Ni ahadi aliyoifanua kuwa pindi wangepatikana wafanyabiashara, ungefanyika utaratibu wa kulipa fidia kwa kaya zote za 'Uwanja wa Fisi', kupageuza kuwa alichokita Dar es Salaam mpya, kuliko eneo hilo lilivyo sasa.

"Mazingira ya 'Mtaa wa Fisi' siyo mazuri. Nimepita, nimejionea mwenyewe baada ya kufanya ukaguzi, nikajiridhisha na hili ndio tamko langu kwa umma kwa wananchi wa mkoa huu," anasema.

Kwa jumla ni kwamba, kumekuwapo ahadi za kuboresha eneo hilo, lakini hakijajulikana kinachokwamisha, hadi kipindi Mkuu wa Mkoa Makonda, ameondoka pasipo kutekelezwa ahadi hiyo.

Wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, mgombea urais kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mgaywa, naye alitua 'Uwanja wa Fisi' akiahidi kupaboresha mazingira yake.

Aliwaachia ahadi kwamba angebadilisha nyumba za eneo hilo na wakapatiwe maghorofa kama ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), ili wanaoishi hapo waondokane na makazi duni, kama njia ya kuboresha maisha ya Watanzania wanyonge.

Kilichoahidiwa na mgombea huyo, ndiyo mzizi wa shauku ya wanaoaka 'Uwanja wa Fisi', kwa kuwa hata Joseph Mkude, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Muungano, ambako 'Uwanja wa Fisi' unapatikana, ndiyo anavyotaka.

Ahadi ni nyingi kwa kweli, lakini mavuno yake ni hesabu finyu. Matamano hayo bado hayajazaa matunda, kutokana na ukweli, maisha ya eneo hilo bado ni yale yale miaka nenda rudi, licha ya kusikika ahadi zisizo hesabika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

Mhariri Mtendaji : Beatrice Bandawe

Meneja Usambazaji na Masoko: Emmanuel Lyimo, 0716 500500

Mapokezi: 0745 700710

Matangazo: 0782 253676

Baruapepe: advertise@guardian.co.tz

Website: www.ippmedia.com

epaperippmedia.com



Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

YETU MICROFINANCE BANK PLC

UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2020 Kiwango kwa Tzs.

| | Robo Mwaka wa sasa 31-Dec-20 TZS | Robo Mwaka Ulipitia 30-Sep-20 TZS |
|--|----------------------------------|-----------------------------------|
| A. MALI | | |
| 1 Fedha Taslimu | 797,494,384 | 721,559,270 |
| 2 Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 119,241,558 | 619,741,826 |
| 3 Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 236,220,305 | 145,738,279 |
| 5 Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | | |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | | |
| 7 Bili Zilizofikiwa | | |
| 8 Dhima za Wateja zilizokubalika | | |
| 9 Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | | |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | | |
| 11 Mikopo Halisi iliyopo | 12,708,353,771 | 12,790,237,905 |
| 12 Mali Nyingine | 1,909,690,719 | 1,626,302,868 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 Akaunti za udhamini | | |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,415,681,723 | 1,827,800,489 |
| 16 JUMLA YA MALI | 1,611,577,911 | 1,424,084,160 |
| | 19,798,260,370 | 19,155,464,797 |
| B. DHIMA | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 Amana za Wateja | 1,845,479,862 | 1,491,323,654 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 Amana Maalumu | 1,743,819,351 | 1,761,759,244 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | | |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | | |
| 24 Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | | |
| 25 Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi | | |
| 26 Mapato yaliyolinga ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 Dhima Nyingine | 480,339,642 | 480,339,642 |
| 28 Madeni | 7,000,000,000 | 7,000,000,000 |
| 29 JUMLA YA DHIMA | 11,069,638,856 | 10,733,422,540 |
| 30 MALI/(DHIMA) HALISI | 8,728,621,515 | 8,422,042,256 |
| C. FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 6,056,496,547 | 6,056,496,547 |
| 32 Akiba ya Mtaji | | |
| 33 Mapato yaliyobakizwa | | |
| 34 Faida/(Hasara) ya Kipindi Husika | 2,213,609,023 | 2,213,609,023 |
| 35 Akaunti zingine za Mtaji | 388,822,945 | 82,243,686 |
| 36 Stahiki ya wenye Hisa chache | 69,693,000 | 69,693,000 |
| 37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA | 8,728,621,515 | 8,422,042,256 |
| 38 Dhima zisizo dhahiri | | |
| 39 Mikopo chechefu | 981,763,273 | 696,959,097 |
| 40 Tongo Kwa ajili ya mikopo chechefu | 749,914,726 | 744,662,234 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | | |
| D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| i Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 44.09% | 43.97% |
| ii Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.29% | 5.15% |
| iii Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 3.75% | 4.16% |
| iv Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 64% | 67% |
| v Uwiano wa Mali Zinzozalisha na Jumla ya Mali | 68% | 71% |
| vi Ongezeko la Amana | 23% | 35% |
| vii Ongezeko la Mali | 3% | 2.63% |

TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2020 Kiwango kwa Tzs

| | Robo Mwaka wa sasa 31-Dec-20 TZS | Robo Mwaka Liganishi 30-Sep-20 TZS |
|---|----------------------------------|------------------------------------|
| I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji: | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 388,822,945 | 82,243,686 |
| Marekebisha kwa Ajili ya: | | |
| - Faida/(Hasara) kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| -Uchakavu wa Mali za Kudumu | (23,474,688) | (27,218,233) |
| -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | - | - |
| -Utumikaji wa Mtaji wa Misada | - | - |
| -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | 365,348,257 | 55,025,453 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | | |
| - Badiliko Halisi katika Mikopo | (283,387,851) | (298,950,221) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (354,156,208) | (367,390,606) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | (37,500,000) | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (309,695,801) | (611,315,374) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - |
| | (309,695,801) | (611,315,374) |
| <i>Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji</i> | | |
| II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | |
| Gawio Liliopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (187,493,751) | (145,778,585) |
| Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| Menginyeo Amana za kudumu | - | - |
| Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | (187,493,751) | (145,778,585) |
| <i>Fedha Halisi Zilizotolewa</i> | | |
| III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha: | | |
| Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| Gawio Liliolipwa kwa Fedha Taslimu | 89,356,219 | (37,807,881) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | 89,356,219 | (37,807,881) |
| <i>Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha</i> | | |
| IV Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu: | | |
| Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha | (407,833,334) | (794,901,840) |
| Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 1,487,039,375 | 2,281,941,215 |
| Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | 1,079,206,041 | 1,487,039,375 |

TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2020 Kiwango kwa Tzs.

| | Kiwango kwa Tzs. (000) | Mtaji wa Hisa | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya jumla | Jumla Tzs |
|---|------------------------|---------------|------------------------|-------------------|--------------------------|-------------------------|------------------|
| Salio la wa mwaka 01/01/2019 | 6,056,497 | 130,555 | - | - | 69,693 | 1,511,458 | 7,768,203 |
| Rekebisha: | | | | | | | |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato mengine | - | - | - | - | - | - | - |
| Mtaji mkuu wa kisheria | - | (130,555) | - | - | - | 130,555 | - |
| Tozo la Mali la mwaka jana | - | - | - | - | - | 433,776 | 433,776 |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | 681,377 | 681,377 |
| Gawio liliolipwa | - | - | - | - | - | (424,817) | (424,817) |
| Salio kwa Mwaka 31.12.2019 | 6,056,497 | - | - | - | 69,693 | 2,332,349 | 8,458,539 |
| Salio la mwaka 01/01/2020 | 6,056,497 | - | - | - | 69,693 | 2,332,349 | 8,458,539 |
| Rekebisha: | | | | | | | |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | - | - | - | - | - |
| Tos: Mapato mengine | - | - | - | - | - | - | - |
| Mtaji wa kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | 322,357 | 322,357 |
| Tos: Gawio liliolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Salio kwa mwaka 31.12.2020 | 6,056,497 | - | - | - | 69,693 | 2,654,706 | 8,780,896 |

